**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

Dodoma, 26, Machi, 2020

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJW) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar inaendelea na juhudi za kudhibiti ugonjwa wa COVID-19 (maarufu kwa jina la Corona) nchini. Hii ni pamoja na kufanya ukaguzi kwa kuwapima joto la mwili (screening) wasafiri wote wanaoingia nchini.

Kuanzia tarehe 1 Januari 2020 hadi sasa jumla ya wasafiri **1,890,532** wamefanyiwa ukaguzi kwa kuwapima joto la mwili (Screening) katika vituo 27 vya mipakani ikiwemo viwanja vya ndege na bandarini. Katika masaa 24 yaliyopita jumla ya wasafiri 3,471 wamefanyiwa screening.

Aidha,Wizara imeendelea kutoa huduma za upimaji wa sampuli za washukiwa wa COVID19 katika Maabara kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii ambapo hadi kufikia Machi 26, 2020, jumla ya watu 273 ( **Tanzania Bara ni 243 na Zanzibar ni 30)** walichukuliwa sampuli za kupima virusi vya Corona. Kati ya sampuli hizo zilizopimwa; 260 hazikuonyesha uwepo wa virusi vya corona, na sampuli za watu **13** zilithibitika kuwa na virusi hivyo. Hivyo hadi sasa tuna jumla ya wagonjwa 13 ambao wamethibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya COVID 19 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mnyumbuliko wa wagonjwa hawa ni kama ifuatavyo:-

Arusha- watu 2

Dar es salaam – watu 8

Zanzibar – watu 2

Kagera – mtu 1

Kupitia taarifa hii, Serikali inapenda kuwapongeza na kuwashukuru watumishi wa sekta ya afya wanaofanya kazi ya kuhudumia washukiwa na wagonjwa wa COVID19 katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma na inawasisitiza kuzingatia taratibu za udhibiti wa maambukizi (Infection Prevention and Control -IPC) wakati wa utendaji wa kazi zao.

Aidha, vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa wa corona (COVID-19) kutoka kwa Wizara ya Afya, kupitia tovuti ya wizara ya afya Msemaji wa Serikali

Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuwasisitizia wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuahirisha safari zisizo la lazima nje ya nchi.

Pamoja na hayo, Wizara inaendelea na jukumu lake la kutoa huduma za afya kwa watu waliothibitika kuwa na ugonjwa wa COVID-19 katika jitihada za kudhibiti maambukizi mapya ya ugonjwa huo nchini. Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia watu wa karibu na wagonjwa (Contact Tracing) hususani katika Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Zanzibar na Kagera

Wizara inapenda pia kutangaza mabadiliko ya namba za simu zinazotumika na wananchi wenye maswali na maoni kuhusu ugonjwa huo, ambapo sasa wanaweza kuwasiliana na si kupitia namba ya bure ya **199** badala ya zilizokuwa zinatumika awali za 0800110037 au 0800110124 au 0800110125.

Taarifa nyingine zinapatikana pia kwenye tovuti yetu; www.moh.go.tz, pamoja na kurasa za Twitter, Instagram na Facebook za Wizara ya Afya, Msemaji Mkuu wa Serikali na kurasa za Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma.

Imetolewa na:

**Ummy A. Mwalimu(Mb)**
**Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**
**26 Machi 2020**

*Wagonjwa hawa raia ni 8 na raia wa kigeni ni 5. Wagonjwa hawa wote 13 isipokuwa mmoja walisafiri nje ya nchi katika siku 14 zilizopita kabla ya kuthibitishwa kuugua, na huyu mgonjwa mmoja alipata maambukizi kutoka kwa mtu aliyekuwa nje ya nchi.* ***Hivyo hadi sasa hakuna maambukizi ya ndani yaani (Local transmission).*** *Wagonjwa wote wanaendelea vizuri. Na leo ninafurahi kuwajulisha kuwa mgonjwa wetu wa kwanza wa Arusha amepona COVID19 na taratibu za kumruhusu kurudi nyumbani zinaendelea, hivyo sasa Arusha inabakiwa na mgonjwa 1.*

Aidha, kuanzia tarehe 23 Machi 2020 abiria wote waliowasili nchini kutoka nchi zilizoathirika zaidi na virusi vya corona wanawekwa karantini ya lazima (mandatory isolation) ya siku 14 katika Hoteli/Maeneo maalum yaliyobainishwa na Serikali, kwa gharama zao. Aidha, tangu kuanza kutekeleza kwa agizo la Mh. Rais jumla ya wasafiri 111 wametengwa kwenye hoteli/maeneo yaliyoandaliwa. Mikoa yote nchini inaelekezwa kuendelea na zoezi la kubainisha sehemu zitakazotumika kuwaweka wasafiri, pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kutekeleza maelekezo haya bila kuleta usumbufu usio wa lazima kwa wasafiri. Hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wasafiri wanamudu gharama zas ehemu husika pamoja na kuhakikisha kuwa Wataalam wa Afya wanaendelea kutoa Ushauri Nasaha (Psychosocial support) kwa wasafiri hao. Hatua hizi zimechukuliwa kwa lengo la kutimiza dhamiria nzuri ya Serikali ya kupunguza hatari ya kusambaa kwa haraka maradhi haya nchini.

Pamoja na jitihada hizo, Wizara ya Afya imepokea msaada wa vifaa tiba kutoka kwaTaasisi zilizoko Jamhuri ya Watu wa China za Jack Ma na Alibaba zilizoshirikiana na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa Ethiopia ili kutoa msaada kwa nchi mbalimbali za Bara la Afrika, ikiwemo Tanzania, kwa ajili ya kuongeza nguvu ya kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19. Miongoni mwa vifaa hivyo vilivyowasili nchini kutoka China kupitia nchini Ethiopia usiku wa Jumanne Machi 24, 2020 ni mavazi maalum ya wahudumu wa sekta ya afya wanapotoa huduma kwa mgonjwa (PPE), "kits" za kupima virusi kwa haraka (Rapid Test Kits), pamoja na Barakoa (masks). Vifaa vilivyopokelewa vitasambazwa kwenye hospitali zilizotengwa maalum kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa mlipuko huu hapa nchini.